**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1105


# Mikakati ya Utetezi wa Mazingira katika Riwaya za *Nakuruto* na *Bustani Ya Edeni*

**Erick Maina[1], Lina Akaka[2] & Rose Mavisi[1]**
[1]*Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Africa Mashariki, Kenya*
[2]*Daystar University, Kenya*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Kupokelewa: 2025-01-18*
*Kurekebishwa: 2025-06-04*
*Kukubaliwa: 2025-06-19*
*Kuchapishwa: 2025-06-24*

***Maneno Muhimu***
Majukwaa
Mazingira
Uhakiki-Ikolojia
Utetezi

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Maina, E., Akaka, L. & Mavisi, R. (2025). Mikakati ya Utetezi wa Mazingira katika Riwaya za *Nakuruto* na *Bustani Ya Edeni*. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *3*(2), 1-9.

*Copyright © 2025*

**Ikisiri**
Makala haya yanalenga kutathmini utetezi wa mazingira katika riwaya za *Nakuruto* (2009) ya Clara Momanyi na *Bustani ya Edeni* (2001) ya Emmanuel Mbogo. Kufuatia uharibifu wa mazingira kote ulimwenguni, utetezi wa mazingira umekuwa ukifanyika katika majukwaa mbalimbali yakiwemo makongamano ya kimataifa, mashirika ya uanaharakati na katika vyombo vya habari. Katika miaka ya hivi karibuni wanafasihi pia wameanza kutumia fasihi kama jukwaa la utetezi wa mazingira katika kazi zao za riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Jambo hili ndilo lililomvutia mtafiti kuchunguza namna suala la utetezi wa mazingira lilivyoshughulikiwa katika riwaya teule. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhakiki-Ikolojia kwa mujibu Glotfelty (1996). Muundo wa utafiti huu ni wa kimaelezo. Sampuli ya utafiti huu ni riwaya za *Nakuruto* (2009) na *Bustani ya Edeni* (2001) ambazo ziliteuliwa kimakusudi ili zichunguzwe. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa mikakati mbalimbali kama vile dini, sheria, vyombo vya habari, mabango, nyimbo na maandamano imetumika kuyatetea mazingira. Makala haya yatawachochea wanaharakati wa mazingira katika kutumia majukwaa mbalimbali kuyatetea mazingira. Aidha, utafiti huu utapiga jeki juhudi za Wizara ya Mazingira katika kuhamasisha jamii kuhusu uharibifu dhidi ya mazingira.

## Utangulizi

Suala la mazingira lilianza kushughulikiwa katika fasihi mwishoni mwa karne ya 18 hadi kati ya karne ya 19 haswa baada ya mfumko wa viwanda na kuongezeka kwa ufahamu wa mazingira (Dilworth, 2007). Wanafasihi wa karne hizo waliangazia masuala ya mazingira katika bunilizi zao. Maandishi ya uhusiano wa fasihi na mazingira yalianza kukita mizizi wakati nadharia ya uhakiki-ikolojia ilipotumiwa katika insha ya Ruekert (1978) kuhusu fasihi na ikolojia, (Buell, 2014). Buell anaeleza kuwa dhana ya uhakiki-ikolojia ilisahaulika hadi mwaka wa 1989 ambapo ilifufuliwa tena katika mkutano wa Chama cha Fasihi ya Kimagharibi. Buell anafafanua kuwa ilipendekezwa kuwa dhana ya uhakiki-ikolojia itumiwe katika kurejelea fasihi na mazingira. Awali, uhakiki-ikolojia ulijulikana kama uandishi kuhusu mazingira. Kimsingi mkabala wa uhakiki-ikolojia uliasisiwa ili kutumia fasihi kushughulikia uharibifu dhidi ya maliasili, athari za mifumo hasi ya kilimo dhidi ya binadamu na uharibifu wa mtandao wa viunga uhai katika fasihi.

Suala hili lilianza kutokea katika uandishi wa waandishi wa Afrika Mashariki miaka michache iliyopita. Kazi inayojulikana ya mapema sana katika fasihi ya Kiswahili iliyoshughulikia suala hili ni ya Mbogo katika riwaya ya *Bustani ya Edeni* (2001), ikifuatiwa na riwaya ya *Nakuruto* (2009) ya

Momanyi. Kazi nyinginezo za fasihi ya Kiswahili za hivi karibuni ambazo zimeshughulikia suala la mazingira ni diwani za mashairi ya Kithaka wa Mberia. Diwani hizo ni *Bara Jingine* (2001), *Redio na Mwezi* (2005), *Msimu wa Tisa* (2007) na *Rangi ya Anga* (2014). Waandishi wengine ambao wamegusia masuala ya mazingira ni Timothy Arege katika tamthilia yake ya *Majira ya Utasa (*2015), Wamitila katika riwaya ya *Tikitimaji* (2013) na *Msimu wa Vipepeo* (2006) na kadhalika. Kazi hizi zimechukua mkabala mpya wa kushughulikia suala hili. Waandishi hawawalaumu Wamagharibi peke yao katika uharibifu wa mazingira. Wanaonyesha kuwa Waafrika pia wana mchango mkubwa katika uharibifu wa mazingira. Hivyo kando na kuonyesha jinsi mazingira yanavyoharibiwa, wanaeleza pia vile yanavyoweza kuhifadhiwa. Ni kwa misingi hii ambapo makala hii inapania kuchunguza vile waandishi wa riwaya za *Nakuruto* (2009) na *Bustani ya Edeni* (2001) wanavyosawiri suala la utetezi wa mazingira.

**Mapitio ya Maandishi**

Nabeta na Ongutte (2014) walichunguza uhusiano kati ya mazingira na mwanawake katika Riwaya ya *Nakuruto (*2009). Walilenga kuonyesha nafasi ya mwanamke Nakuruto katika kuhamasisha jamii kuhusiana na uharibifu wa mazingira. Nabeta na Ongutte (2014) wanasema kuwa mhusika Nakuruto katika riwaya hii anasukumwa na sheria za Mkutano wa *United Nations Framework Convention on Climate Change* Umoja wa Mataifa wa (UNFCC ,2009) ya uwajibikaji wa pamoja ambayo msingi wake ni asasi za kitamaduni. Wanakubaliana na Moore (2008) kuhusu kuwapo na uhusiano wa moja kwa moja kati ya mazingira na mwanamke.

Utafiti wa Nwagbara (2010) unaeleza jinsi waandishi nchini Nigeria walivyotumia fasihi kuhamasisha jamii kuhusu uharibifu wa mazingira na athari yake kwa maisha ya binadamu. Nwagbara aliangazia mashairi ya Ojaide ya *Delta Blues and Home Songs (*1998) na *Daydreams of Ants and Other Poems (*1997) ambayo yanalenga kuelezea uharibifu wa mazingira katika eneo la Delta nchini Nigeria.

Sabula (2014) ameangazia nafasi ya mwanamke katika uhifadhi wa mazingira kwenye riwaya ya *Nakuruto* (2009) huku akijikita katika mtazamo wa ufeministi wa kiikolojia. Katika utafiti wake, Sabula (2014) aliongozwa na mihimili ya nadharia ya ufeministi wa kiikolojia. Anaonyesha nafasi na mchango wa ufeministi wa kiikolojia katika fasihi ya Kiswahili. Vilevile, anaonyesha juhudi za Nakuruto kama mhusika wa kike katika hali ya kupigania uhifadhi wa mazingira. Isitoshe, katika utafiti wake, anaonyesha kuwa ufeministi wa kiikolojia una mchango mkubwa katika kuwazindua wanawake ili kuleta ukombozi wa mazingira. Ameonyesha jinsi mhusika Nakuruto anavyoelimisha jamii kuhusu athari za mabadiliko ya anga na jinsi wanavyoweza kujinasua kutokana na hali hii. Pia, anaonyesha jinsi mwanamke anavyodhulumiwa na kudhihakiwa anapojaribu kujihusisha na harakati za uhifadhi wa mazingira. Pia, amebainisha jinsi masuala kama vile umasikini, kukauka kwa chemchemi za maji, maradhi na mauti yanavyosababishwa na uharibifu wa mazingira.

Bulaya na Mhango (2019) walichunguza ujitokezaji wa maudhui ya utunzaji wa mazingira katika hadithi teule za watoto: *Kavuta Mrina Asali* (2006), *Mbawala na Nchi ya Ujinga* (2006), *Mtoto Mrembo (*2006) na *Watoto Wanaofanana* (2006). Katika utafiti wao walibaini kuwa mapambano dhidi ya uharibifu wa mazingira ni shirikishi bila kujali jinsia, umri, elimu, hali ya ulemavu, mamlaka au uwezo wa kiuchumi alionao mtu.

Njeru (2020) alichunguza motifu ya ukame katika Tamthilia za *Janga la Werevu* (2011) na *Majira ya Utasa* (2015). Njeru alilenga kujadili namna watunzi wa tamthilia za *Janga la Werevu* (2011) na *Majira ya Utasa* (2015) wamesawiri motifu ya ukame kama suala mojawapo la kimazingira kwa lengo la kuweka wazi chanzo na athari zake katika jamii. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kuwa ukame unaweza kusababishwa na mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la joto duniani, hali ya kuasi baadhi ya

mambo ya jadi na ukataji wa miti. Vilevile, ilidhihirika kwamba, ukame ulisababishwa na tamaa ya viongozi iliyowafanya wajihusishe katika unyakuzi wa ardhi pamoja na kuharibu vyanzo vya maji. Aidha, ilibainika kwamba hali ya ukame huwa na athari nyingi kama vile kukauka kwa mimea, uhaba wa chakula, umaskini, kudidimia kwa maliasili na kuathirika kwa masomo.

Wasonga, Ambuyo na Mzungu (2020) walichunguza nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya mazingira kupitia kwa riwaya za Wamitila; *Tikitimaji* (2013) na *Msimu wa Vipepeo* (2006). Utafiti wao ulibaini kuwa fasihi ni nyenzo mwafaka ya kuwasilisha masuala ya mazingira kupitia vipengele vyake kwani huingiliana sana na utamaduni wa jamii.

Mosha (2023) alichunguza dhima ya nyimbo za Kiswahili za watoto katika kujifunza mazingira. Alichunguza mchango wa fasihi ya Kiswahili hususani nyimbo za watoto, nchini Tanzania katika taaluma ya mazingira. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa nyimbo za Kiswahili za michezo ya watoto ni muhimu kwa watoto na jamii, si tu katika kujifunza mazingira ya jamii mahususi, bali pia katika kuwasilisha maudhui yahusuyo mazingira kwa jamii pana.

**Misingi ya Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhakiki-ikolojia iliyoasisiwa na Glotfelty (1996). Katika kazi yake ya *Ecocriticism Reader*, Glotfelty anaeleza kuwa uhakiki-ikolojia ni uchunguzi wa uhusiano baina ya fasihi na mazingira ya kiasili. Anasisitiza kuwa uhakiki-ikolojia huchanganua vile mazingira ya kiasili yanavyowakilishwa katika fasihi na vile fasihi husaidia kuunda uelewa wa mazingira. Glotfelty anasema kwamba kwa muda mrefu, mazingira yalipuuzwa na fasihi kama taaluma ambayo ingefanyiwa uchunguzi.

Kwa mujibu wa Sunday (2018), waendelezaji wa nadharia hii katika majukwaa ya mijadala, fasihi na miktadha mbalimbali ya kimazingira ni pamoja na Harold Fromm, Lawrence Buell, Simon Estok, William Howarth, Joseph Meeker, Christopher Manes, Neil Evernden, David Mazel, Scott Slovic, Ursula Heise, Karen Thornber, Thomas Lyon, Sueellen Campbell, Tawi la Michael, Lawrence Coupe, Kate Rigby na Glen Love. Glotfelty na Harold (1996), Greenblatt (1992), Buell (1995) wanaeleza kuwa nadharia ya uhakiki-ikolojia huangalia mielekeo ya binadamu kuhusu mazingira. Mielekeo hii ni pamoja na matumizi ya dhana za ekolojia katika kazi za fasihi, nguvu za kibinadamu na lugha ya binadamu kuhusiana na mazingira, mitindo ya lugha na jinsi mitindo hiyo huathiri namna binadamu anavyotagusana na mazingira. Kulingana nao nadharia hii huchukulia kwamba mazingira na utamaduni hushirikiana hivi kwamba binadamu hawezi kuishi bila ekolojia lakini ekolojia huweza kuishi bila binadamu. Naye Rigby (2007) anaeleza kuwa nadharia hii imejitokeza kubadili hali halisi ya uharibifu wa ekolojia kwa kuchanganua uamilifu wa kimaudhui, kisanii, kijamii, kihistoria, kiitikadi na kimbinu katika ekolojia asilia au vipengele vyake kama vinavyohusishwa katika fasihi. Makala ya Rueckert (1978) ya *Literature and Ecology: An Experiment in Ecocriticism* yaliweka misingi katika nadharia hii. Mhimili wa nadharia ya uhakiki-ikolojia wa mazingira yana haki ya kutetewa na wanajamii kama suala la kijamii hususan matatizo ya kimazingira yanayozikumba jamii za mataifa yanayoendelea. Kulingana na mhimili huu, wanaokubaliana na mawazo ya uhakiki-ikolojia wana jukumu la moja kwa moja au lisilo la moja kwa moja la kutekelezaili kuyatetea mazingira. Mhimili huu uliwawezesha watafiti kutathmini jinsi utetezi wa mazingira ulivyojitokeza katika riwaya za *Nakuruto* na *Bustani ya Edeni*.

**Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Muundo wa kimaelezo ni njia ya kukusanya data na kuzifanyia uchambuzi kwa njia ya kimaelezo ambapo nambari huwa hazitumiki (Enon, 1998). Hivyo, data za utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa njia ya maelezo. Eneo la utafiti la utafiti huu

ni riwaya ya Kiswahili. Kundi lengwa katika utafiti huu ni riwaya ya Kiswahili. Sampuli ya utafiti huu ni riwaya mbili; riwaya ya *Nakuruto* (2009) na *Bustani ya Edeni* (2001). Riwaya hizi ziliteuliwa kimakusudi kwa sababu zinaangazia masuala ya kimazingira, haswa utetezi wa mazingira. Data ilikusanywa kutoka riwaya mbili; *Nakuruto* (2009) na *Bustani la Edeni* (2001). Data za msingi zilikusanywa kupitia usomaji makini wa riwaya teule zaidi ya mara moja. Mtafiti alikusanya data za utafiti kwa kutumia kalamu na daftari kutoka katika riwaya teule zilizochunguzwa. Data ilipangwa katika mada ndogondogo zilizohusiana na lengo la utafiti na kuwasilishwa kimaelezo.

**Mikakati ya Utetezi wa Mazingira katika Riwaya ya *Nakuruto* na *Bustani ya Edeni***

Utetezi wa mazingira unajumuisha juhudi na mikakati mbalimbali inayofanywa na watu binafsi au vikundi ili kushawishi sera za umma na maamuzi ya mgao wa rasilimali ndani ya mifumo na taasisi za kisiasa, kiuchumi, na kijamii. Juhudi hizi zinaweza kujumuisha elimu, ushawishi wa kisiasa, kampeni, na aina mbalimbali za harakati. Utetezi wa mazingira ni muhimu kwa kulinda ardhi yetu, maji, na wanyamapori. Katika enzi hizi ambazo changamoto za kimazingira zimeenea na watu wanakumbana na athari za ongezeko la joto duniani, ukame, mafuriko pamoja na changamoto zingine zitokanazo na uharibifu wa mazingira, fasihi mazingira inayohusu kazi za fasihi zinazoangazia masuala ya mazingira na uhusiano wa binadamu na mazingira ya asili imekuwa jukwaa muhimu ya kutetea mazingira. Kupitia simulizi za kuhamasisha fikra, fasihi mazingira ina uwezo wa kubadili mitazamo yetu kuhusu mazingira, kuhamasisha watu kuchukua hatua, na kuunda mustakabali endelevu. Katika kuyatetea mazingira, waandishi wa riwaya teule wametumia mikakati mbalimbali kama vile uzinduzi, ukombozi, dini, vyombo vya habari, sheria, mabango na nyimbo katika kuyatetea mazingira.

**Mbinu ya Uzinduzi katika Utetezi wa Mazingira**

Mbinu hii inahusisha uhamasishaji tofauti na mbinu anayoishabikia Glotfelty (1996), mbinu ya kuyatetea mazingira kupitia kazi andishi za fasihi. Hata hivyo lengo kuu la mbinu yoyote ile ni kuhamasisha jamii. Katika riwaya ya *Nakuruto* mhusika Nakuruto anawazindua wanavijiji wa Latimbi, Maweni na Maboni kuwa kuna uhusiano kati ya ukosefu wa miti na kukauka kwa vyanzo vya maji. Anawaeleza kuwa kila tone la mvua linaloanguka huingia ardhini hadi kwenye vihifadhi vya maji vilivyopo ardhini na ndivyo chemichemi ya vyanzo vilivyoko kwenye ardhi. Wanakijiji hawa hawakufahamu uhusiano huu. Hawakujua kiasi gani walitegemea mfumo wa ekolojia na hivyo walikata miti na kuharibu maeneo oevu kwa manufaa yao wenyewe kiuchumi. Nakuruto anawazindua wanakijiji kwa lengo la kurejesha mfumo wa ekolojia kwa upanzi wa miti, kuondoa wanyonyaji ardhi na sera zao za ukoloni. Katika ukingo wa ziwa Ipe, Nakuruto anagundua hatari iliyokuwa inawachungulia wanakijiji kutokana na uharibifu wa mazingira ya ziwa. Aliwazindua ili kufahamu haja ya kulinda hili ziwa. Anawauliza:

> … Chanzo cha uhai wenu ni Ipe, nanyi mko mbioni kuukatiza. Je, mtoto mchanga akikatiziwa ziwa la mamaye hatotishiwa uhai wake? Fikiria jibu la swali hili. (uk 32)

Usemi huu unaonyesha kuwa wanakijiji hawakuwa na ufahamu kuhusu kile kinachositiri uhai wao, hali ambayo inawafanya waendeleze uharibifu wa mazingira kwenye ziwa. Nakuruto anatoa ilani na kuwaomba kupitisha ujumbe huo ili kuibuka na mikakati ya kulinda ziwa. Mama Bintifundi (uk 36) anakubaliana na uzinduzi wake Nakuruto.

Nakuruto kama mzinduzi kwa masuala ya kimazingira, anaendelea kujitokeza katika kila kijiji kama mtaalamu wa mazingira. Analinganisha mazingira na elementi za binadamu katika shughuli zake za kuzindua wanavijiji. Analingananisha maji kama pumzi ya uhai na ardhi kama kitovu cha uhai,

inapobusiwa na jinsi huchipua uhai (uk 28). Anaona ardhi isiyo na maji kama mzazi aliyepokwa uwezo wa kuendeleza kizazi chake (uk 105).

**Ukombozi katika Utetezi wa Mazingira**

Mbinu ya ukombozi wa mazingira ni juhudi zinazolenga kukomesha uharibifu wa mazingira ili binadamu afurahie ekolojia yake. Kwa mfano, katika riwaya ya *Nakuruto*, Nakuruto anasimama imara na wanavijiji mbalimbali katika juhudi za kuhakikisha kwamba uharibifu wa mazingira umepungunzwa na hata kukomeshwa ili wanavijiji wafurahie mazingira yao. Nakuruto anatumia wito wa ukombozi katika harakti ya kuyakomboa mazingira. Anapanga kuondoa Bwana Brook katika mashamba ya Walatimbi ili kuikomboa ardhi yao. Anashauri umati ulivamie kasri na hata kulichoma ili Brook asipate nafasi ya kurudi tena. Katika kumuondoa Brook wangeweza kukomboa mashamba yao na kuimarisha hali yao ya shibe majumbani mwao. Nakuruto anawaambia Walatimbi:

> … Mkifaulu kumwondoa haini yule katika ardhi yenu, jigawanyieni mashamba ambayo ni haki yenu mliyoridhi kutoka kwa mababu zenu. Kuzeni mazao ya kila aina wana wenu. Bila kukita mizizi sawasawa katika ardhi yenye rutuba, makuunga na matagaa hunyauka na uhai kupotea. Fahamuni hili. (uk 44-45)

Nakuruto anafanikiwa kutumia mbinu ya ukombozi kuleta mabadiliko ya kimazingira. Anawachochea wanyonge kubadilisha hali zao kwa kupindua utawala katili kwa ajili ya mazingira yao, mustakabali na watoto wao ili hali iwe kama ilivyokuwa enzi za mababu zao.

**Dini katika Utetezi wa Mazingira**

Glotfelty (1996) anazungumzia nafasi dini kama sehemu muhimu ya utamaduni ambao una ushawishi mkubwa katika jinsi jamii zinavyotazama na kuhusiana na mazingira. Ingawa hakuandika moja kwa moja kuhusu dini kwa undani, kazi yake inaonyesha kuwa mifumo yote ya imani na falsafa, ikiwemo dini, lazima izingatiwe katika kuelewa na kutetea mazingira. Katika riwaya ya *Bustani ya Edeni*, dini ina mchango mkubwa katika kuyatetea mazingira kupitia kiongozi wake Pasta Yona. Huyu ni mhubiri ambaye anatumia dini kukemea uchafuzi wa mazingira. Anaungana na Jonalisti, na Mwanasheria Wakili Mwaka na wanajamii kutetea mazingira na anatumia nafasi yake kama kiongozi wa dini na ushawishi alionao kuwafunza waumini na wasio waumini wake madhara yanayotokana na uchafuzi wa mazingira.

Kutokana na msimamo na juhudi zake za kutetea mazingira Pasta Yona anachaguliwa na viongizo wa dini kuwasilisha maazimio yao kuhusu mazingira ya mji wa Siza kwa Waziri wa Viwanda kupitia barua. Pasta Yona anachaguliwa kwa sababu yeye ndiye kiongozi wa dini aliyepinga sana uchafuzi wa mazingira uliofanywa na kiwanda cha Sagasaga kuliko kiongozi mwingine yeyote wa dini hata siasa (uk 33). Anaapa kuchukua hatua ya kufunga na kuitisha mgomo na maandamano ya Wanasiza wote dhidi ya kiwanda cha Sagasaga kama serikali haitachukua hatua (uk 45).

Katika mahubiri yake kuhusu Dunia na Binadamu (uk 75) anawaonyesha waumini wake jinsi Bustani ya Edeni ambayo binadamu alizawadiwa na Mwenyezi Mungu katika kitabu cha Mwanzo ambayo ilijaa wanyama na ndege wa kuvutia, Bustani iliyokuwa na miti na maua, mabonde na milima ya kupendeza imeharibiwa na binadamu kwa kisingizio cha maendeleo na sayansi na teknolojia.

**Vyombo vya Habari katika Utetezi wa Mazingira**

Vyombo vya habari ni muhimu katika usambazaji wa taarifa mbalimbali zikiwepo za mazingira. Oduor (2016) anasema kuwa vyombo vya habari hutekeleza jukumu la kimsingi katika kutoa habari vikiwa na lengo la kuhamasisha jamii kuhusu masuala muhimu. Vyombo vya habari vimetumika kutetea mazingira hususani magazeti katika riwaya ya *Bustani ya Edeni*. Jonalisti

ametumia vyombo hivi kuhamasisha jamii kuhusu uharibifu wa mazingira. Jonalisti ni mwandishi wa habari, jina lake halisi ni Daudi Samora. Anatumia vyombo vya habari kufichua uchafuzi wa mazingira unaofanywa katika mji wa Siza na kuyachapisha katika gezeti la Kiswahili, *Jamii Yetu* na gazeti la Kiingereza, *Our Society* (uk 15). Anatumia taaluma yake kutafuta habari kuhusu uchafuzi wa mazingira na kuandika makala katika gazeti kuhusu masuala ya mazingira kwa ujumla.

Baada ya Eliya na wenzake kulazwa katika hospitali ya wilaya ya Siza, Jonalisti anawatembelea na anatumia fursa hiyo kuwahoji kuhusu yalitokea kiwandani na kunakili yote yaliyosemwa kwa hati ya mkato kwenye daftari lake. Anelekea kiwandani Sagasaga ili kupata habari zaidi kuhusu kashfa ya ajali ya wafanyakazi kiwandani Sagasaga. Alilenga kutumia habari hizi ili kuwatikisa matajiri wa Sagasaga na uchafuzi wa mazingira kwa kutumia magazeti yao ya kila siku kwa lugha ya Kiswahili, *Jamii Yetu* na la Kiingereza, *Our Society* (uk 15-16).

Katika vita kubwa dhidi ya uharibifu wa mazingira kupitia maandamano, anachukua jukumu la kurekodi matukio yote kupitia upigaji picha na uandishi wa habari wa matukio yote. Miongoni mwa picha alizopiga ni zile za waandamanaji waliobeba mabango yenye jumbe mbambali kama vile viwanda visivyofuata sheria za Shirika la Afya Duniani (WHO*)* kufungwa, Sagasaga kama sumu kwa maisha ya Wanasiza, upingaji wa umwagaji wa takataka za nyuklia katika mji wa Siza na kadhalika. (uk. 89-90). Hata hivyo maandamano haya ya kupinga kuwepo kiwanda cha Sagasaga yalirekodi takriban vifo vya watu hamsini. Kutokana na hali hii Rais anaamuru kufungwa kwa kiwanda cha kemikali cha Kampuni ya *Cel* kilichoko Siza. Kiwanda ambacho kwa muda mrefu kiliendeshwa na kuzalisha kemikali mbalimbali bila kufuata masharti na kanuni za *WHO* zinazohusu uchafuzi wa mazingira. Vyombo vya habari hususani gazeti katika riwaya hii ya *Bustani ya Edeni* ni silaha muhimu katika upatikanaji wa haki ya mazingira kupitia makala ya Jonalisti. Anasukumwa na sheria ya *UNFCC* (2009) ya uwajibikaji wa pamoja ambayo msingi wake ni asasi za kitamaduni. Anakubaliana na Moore (2008) kuhusu kuwapo na uhusiano wa moja kwa moja kati ya mazingira na binadamu. Hivyo anayabaini haya kupitia makala yake magazetini.

**Mabango katika Utetezi wa Mazingira**

Glotfelty (1996) anaamini kuwa maandishi yote yakiwemo mabango yana uwezo wa kuwasilisha ujumbe kuhusu masuala ya mazingira. Matumizi ya mabango ni mbinu mojawapo ambayo imetumika katika utetezi wa mazingira katika riwaya ya *Bustani ya Edeni*. Katika maandalizi ya maandamano ya kupinga kuwepo kwa kiwanda cha Sagasaga, Pamela alikuwa na jukumu la kuandika mabango na maberemu yatakayobebwa na waandamanaji (uk. 74). Wakati wa maandamano (uk. 87-90) watu walibeba mabango yaliyokuwa na ujumbe mbalimbali wa kutetea mazingira. Kwa mfano bango moja lilikuwa na maandishi yafuatayo;

"… GESI YA SAGASAGA NI SUMU KWA MAISHA YETU" (uk. 89)

Bango hili linatokana na matatizo ya kiafya wanayokumbana nayo Wanasiza kutoka na gesi ya Sagasaga hususani vikohozi visivyoisha, mvua ya asidi pamoja na kuwepo kwenye hatari ya kupatwa na saratani. Linahamasisha kwamba gesi ya Sagasaga sio salama kwa afya za Wanasiza kwani ni sumu.

"… KATA MITI, PANDA MITI" (uk. 90)

Maneno ya bango hili yaliwaonya waliokata miti ovyo misituni kwa ajili ya kuni au mbao. Jonaliti anakubaliana na Pamela katika makala yake kuwa kupigania usafi wa mazingira sio tu kupambana na matajiri wa viwanda bali pia kutokata miti ovyo na kuchoma nyasi ovyo hasa wawindaji na wakulima. Jonalisti anasizitiza kuwepo na haja ya kupanda miti na nyasi ili kuyatunza mazingira.

**Sheria katika Utetezi wa Mazingira**

Sheria ni kanuni zinazowekwa katika nchi ili kutoa mwongozo wa jinsi ya kutekeleza mambo kwa usahihi. Sheria lazima zifuatwe na watu wote, na anayevunja sheria huadhibiwa. Sheria ni mfumo wa kijamii unaoakisi mtazamo wa jamii kuhusu mazingira (Glotfelty, 1996). Kwa mfano, katika riwaya ya *Bustani ya Edeni* sheria imetumika kupitia kwa Mwaka, wakili ambaye ni profesa wa sheria katika Chuo Kikuu cha Nomila katika kuyatetea mazingira. Anajulikana kwa sababu kila mara alijitolea kuwatetea mahakamani wafanyakazi na wakulima wa kawaida waliokuwa wakionewa na kudhulumiwa haki zao na matajiri ama hata serikali (uk. 50).

**Nyimbo katika Utetezi wa Mazingira**

Katika riwaya ya *Bustani ya Edeni*, nyimbo zimetumiwa kuhamasisha kuhusu uharibifu wa mazingira unaofanywa na Abdula na kiwanda chake cha Sagasaga. Mama Mohamed anakiri kuwepo kwa nyimbo za kumtukana Abdula na *Cel* (uk 68). Pasta Yona, Jonalisti, Wakili Mwaka, Eliya, Pamela, Dorcas, Mama Mohamed, Kapteni, Samsoni na wengine walipokuwa wakiendelea na mkutano wa kujiandaa na maandamo, kundi la wachezaji ngoma wanajiunga nao kwenye kikao kwa kucheza densi, ngoma, na kuimba. Waliimba wimbo wa Abdula na *Cel,* wimbo ambao uliwasisimua Pasta Yona, Pamela, na Wakili Mwaka kuwafanya kujiunga nao kucheza (uk 68-69). Wimbo huu unahusu matokeo ya uchafuzi wa mazingira katika Siza. Unathibitisha kuwa mazingira yamechafuliwa na matokeo yake ni kuwa Wanasiza wana vidonda, wanapunyuka nywele, wanajikuna mwili mzima, na wanatokwa na kamasi. Kulingana na kibwagizo matatizo haya yalisababishwa na *Cel,* Abdula, gesi, na pesa. *Cel* ni kiwanda cha Sagasaga. Wimbo huu uliendelezwa kwenye maandamano ya Juni 5, ujumbe kwenye kibwagizo ukiongezeka. Abdula anachorwa kama mlaumiwa wa matatizo yote ya Wanasiza ikiwemo uchafuzi unaofanywa na dampu la Siza. (uk. 87-88)

Kilele cha utetezi huu wa mazingira ni maandamano ambayo yalihusisha wanaharakati Pasta Yona, Jonalisti, Wakili Mwaka, Pamela, Dorcas, Mama Mohamed, Kapteni, Samson, Eliya, na Wanasiza wote. Hii ni baada ya Pasta Yona, Jonalisti, Wakili Mwaka na Pamela kutumia taaluma zao kama majukwaa ya kutetea mazingira. Katika maandamano haya vifo vipatavyo hamsini vinarekodiwa baada ya polisi kuwafyatulia risasi waandamanaji. Miongoni mwa wanaharakati waliofariki katika maandamano hayo ni pamoja na Dorcas, Pamela na Pasta Yona ambaye aliuawa asubuhi ya siku ya maandamano na mwili wake kupatikana malishoni na mtoto Metu. Ripoti ya shirika la kimataifa la *Global Witness* iliyochapishwa Septemba 2024 inasema kuwa mwaka wa 2023 takribani wanaharakati 200 wa mazingira waliuawa duniani kote. Kwa mujibu wa Laura Furones, mwandishi wa ripoti hiyo, kadri mzozo wa mabadiliko ya tabia nchi unavyoongezeka ndivyo wale wanaotumia sauti zao kwa ujasiri kutetea sayari yetu wanakabiliwa na ukatili, vitisho na mauaji. Kulingana na ripoti hiyo, wanaharakati wanaofanya kampeni dhidi ya uchimbaji madini, uvuvi, ukataji miti, kilimo biashara, barabara na ujenzi wa miundombinu na mitambo ya kuzalisha umeme wanaishi kwa hatari. Furones anasema serikali hazipaswi kufumbia macho ukatili wanaopitia watetezi wa mazingira, bali zinafaa kuchukua hatua za kuwalinda watetezi wa mazingira na kushughulikia sababu zinazochangia ukatili huo.

**Hitimisho**

Tathmini ya utetezi wa mazingiria katika riwaya za *Nakuruto* na *Bustani ya Edeni*, imebainisha kuwa mbinu mbalimbali kama vile uzinduzi, ukombozi, dini, maandamano, sheria, vyombo vya habari, mabango na nyimbo zimetumika kayatetea mazingira. Mbinu hizi zimebuniwa kutokana na hali kwamba binadamu ameharibu mazingira yake bila kujali matokeo yake. Kufuatia hali ya uharibifu wa mazingira, watafiti wanapendekeza majukwaa ya uanaharakati na kijamii yatumike kuyatetea mazingira. Kwa kutumia teknolojia ya kidijitali na mitandao ya kijamii, wanaharakati wanaweza

kufikia hadhira kubwa, kuhamasisha jamii, na kushinikiza mabadiliko ya sera na tabia zinazolinda mazingira. Majukwaa ya kijamii kama vile *Facebook, Instagram*, na *TikTok* yanaweza kutumika kuanzisha kampeni za utetezi wa mazingira, kusambaza habari, na kuhamasisha watu kushiriki. Watafiti wanapendekeza pia ujumuishwaji wa suala la mazingira katika akili unde na teknolojia nyinginezo ili maarifa kuhusu malezi ya mazingira yawafikie watu wengi. Hii ni kwa sababu akili unde imekuwa sehemu ya utamaduni, imeanza kutumika katika shughuli mbalimbali kama vile kwenye sekta ya afya, elimu, dini, usafiri na kadhalika. Vile vile Serikali kupitia kwa wizara ya mazingira inaweza kutenga angalau siku moja ya kila mwezi kama vile jumamosi ya mwisho wa mwezi kama siku ya usafi wa mazingira kwa wote. Katika siku hii, watu wanapaswa kufanya usafi wa mazingira yao hususan sehemu ambazo hazipati kufanyiwa usafi wa mara kwa mara kama vile mitaani kupitia ufagiaji na huokotaji wa taka na kuzichoma katika sehemu maalum. Usafishaji wa mito na upandaji wa miti unaweza kufanywa pia katika siku hii. Watakaokosa kushirika katika zoezi hili watozwe faini kali. Ufanisi wa mpango huu unaweza kufanywa kupitia kwa serikali za mitaa.

## Marejeleo

Bennett, A. J. (1991). Agrarian politics and the economics of writing: Keats's "To Autumn". *Criticism, 33(3),* 333–352.

Buell, L. (1995). *The Environmental Imagination: Thoreau, nature writing, and the formation of American culture.* Cambridge University Press.

Bulaya, J., & Mhango, P. (2019). Ujitokezaji wa Maudhui ya Utunzaji wa Mazingira katika Hadithi Teule za Watoto: Mifano kutoka Fasihi ya Kiswahili. *Mulika no. (38)*, 105 -125.

Dilworth, T. (2007). Parallel Lights in Coleridge's 'The Rime of the Ancient Mariner'. *Explicator, 65*(4), 21-215.

Enon, J. C. *(1998). Education research, statistics, and measurement.* Makerere University Press.

Glotfelty, C., & Fromm, H. (1996). *The Ecocriticism Reader: Landmark in Literary Ecology.* University of Georgia Press.

Glotfelty, C. (1996). *The Ecocriticism Reader: Landmarks in Literary Ecology*. University of Georgia Press.

Greenblatt, S. (1992). *Marvellous Possessions: The wonder of the New World*: Chicago University Press.

Mbogo, E. (2001). *Bustani ya Edeni*. Longhorn Publishers.

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto*. Longhorn Publishers.

Moore, N., 2008. Eco-Feminism, Non-violence and the Future of Feminism. *International Feminist Journal of Politics 10*(3), pp.282–98.

Mosha, D., & Omari, S. (2020). Dhima ya Nyimbo za Kiswahili za Watoto katika Kujifunza Mazingira. *Kioo cha Lugha*, *20*(2), 184-197.

Nabeta, S., & Ongutte, R. (2014). "Literary environmentalism: An ecocritique of Kiswahili Literature." *International Journal of Ecology and Ecosolution vol. 1*(2), 29- 41,

Njeru, M. K. (2020). Motifu ya Ukame katika Tamthilia za Janga la Werevu (Mohamed, 2011) na Majira ya Utasa (Arege, 2015). *East African Journal of Swahili Studies, 5*(1),183-195. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.733

Nwagbara, U. (2010). Poetics of resistance: Ecocritical reading of Ojaide's poems *Delta Blues and Home Songs* and *Daydream of Ants and Other Poems*. *African Study Monographs*, *31*(1), 17–30.

Oduor, J. A. (2016). *An Analysis of Kenya`s Mainstream Print Media`s Usage of Objectification and Anchoring to represent the Kenyan International Crimnal Court Cases in the Daily Nation and the Standard News Articles*. MA Thesis, Maseno University, Unpublished.

Rigby, K. (2007). *Ecocriticism: Introducing Ecocriticism in the Twenty-first Century*. Edinburgh: UP.

Rueckert, W. (1978). Literature and ecology: An experiment in ecocriticism. In C. Glotfelty & H. Fromm (Eds.) *The ecocriticism reader: Landmarks in literary ecology* (pp. 105–123). University of Georgia Press.

Sabula, A. M. (2014). *Nafasi ya Mwanamke katika Uhifadhi wa Mazingira katika Riwaya ya Nakuruto: Mtazamo wa Fasihi ya Ufeministi wa Kiekolojia* [Unpublished master's thesis]. Chuo Kikuu cha Nairobi. https://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/75733?show=full

Sunday, Y. D. (2018). *Modern Nigerian fiction and the rhetoric of eco-culture: An ecocritical reading of Adamu Kyuka Usman's The Death of Eternity, Tanure Ojaide's The Activist and Kaine Agary's Yellow Yellow* [Unpublished seminar paper]. Department of English and Literary Studies, Ahmadu Bello University, Zaria.

UNFCC. (2009). *Decisionx.CP.15Methodological guidance for activities relating to reducing emissions from deforestation and forest degradation and the role of conservation, sustainable management forests and enhancements of forests carbon stocks in developing countries.* FCC/CP/2009/11Add.1, decision4/CP.15. http://unfccc.int/files/na/application/pdf/cop15_ddc_auv.pdf. Accessed 07/08/2017.

Wesonga, E., Ambuyo, B., & Mzungu, R. (2020). Nafasi ya Fasihi Katika Kuwasilisha Masuala ya Mazingira Kupitia Riwaya Teule Tikitimaji (2013) na Msimu wa Vipepeo (2006) za K. W. Wamitila. *East African Journal of Swahili Studies, 2(2)*, 54-64. https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.192